MAELEKEZO YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KUHUSU MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA KWA MWAKA 2020

Awali ya yote, natumia fursa hii kuungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyetuwezesha kupambana na Ugonjwa wa Homa Kali ya Mapafu unaosababishwa na Virusi vya Corona (COVID-19) na hatimaye kuendelea na shughuli za ujenzi wa taifa.

Ofisi yangu kama ilivyo kawaida ya kila mwaka, imekuwa na utaratibu wa kuzitaarifu taasisi zote za umma namna ya kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma kwa mwaka husika.

Ninapenda kutumia fursa hii kuwapongeza Watumishi wa Umma wote nchini kwa kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi na wadau, licha ya kuwepo na changamoto ya ugonjwa wa Homa Kali ya Mapafu unaosababishwa na Virusi vya Corona nchini.

Kabla sijazungumzia Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2020, ni vema tukakumbushana japo kwa ufupi historia ya Siku ya Utumishi wa umma Barani Afrika.

Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika ni siku maalum ya Watumishi wa Umma ambayo husherehekewa tarehe 23 Juni kila mwaka na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) kwa lengo la kutambua mchango wa Watumishi wa Umma katika maendeleo ya nchi zao na Bara la Afrika kwa ujumla. Chimbuko la sherehe hizi ni uamuzi wa Mkutano wa Mawaziri wenye dhamana ya Utumishi wa Umma uliofanyika Tangiers Nchini Morocco mwaka 1994. Uamuzi huu ulizitaka nchi za Afrika kusherehekea siku hii kwa kauli mbiu moja katika Bara zima la Afrika.

Aidha, Mkutano wa nne wa Mawaziri wenye dhamana na Utumishi wa Umma uliofanyika Mwezi Mei 2003 uliamua kuwa Siku ya Utumishi wa Umma iwe ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Utawala Bora na Utumishi wa Umma chini ya Umoja wa Afrika (AU).

malengo na faida ya Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika ni haya yafuatayo;

i. Kutambua mchango na umuhimu wa Watumishi wa Umma kuleta maendeleo katika mataifa yao ili kutoa motisha na ari ya utendaji kazi kwa watumishi wa umma.

ii. Kuwezesha watumishi wa umma kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Dira, Dhima, Malengo, Programu na Mikakati kwa lengo la kutoa huduma kwa umma.

iii. Kuhamasisha na kuwapa motisha Watumishi wa Umma waendelee na kazi ya ujenzi wa Taifa na kuwa wabunifu katika kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii.

iv. Kupata mrejesho kutoka kwa wateja/wananchi na wadau wanaohudumiwa ili kurekebisha kasoro za utendaji zinazosababisha malalamiko ya wateja dhidi ya huduma zinazotolewa na taasisi za umma.

Ninaomba sasa nizungumze Maadhimisho ya Siku ya Utumishi katika ngazi ya Taifa kwa mwaka 2020;

Hapa nchini, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora huratibu maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kitaifa.

Kauli Mbiu ya Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka 2020 iliyotolewa na Umoja wa Afrika (**AU**) kupitia taarifa yake (**Note Verbale**) kwa lugha ya kiingereza ni ***“The Role of Public Administration in***

Building and Sustaining Peaceful Co-existance Among Communities*"* na kwa tafsiri ya kiswahili ni;

"Jukumu la Utumishi wa Umma katika Kujenga na Kudumisha Amani iliyopo Miongoni mwa Jamii."

Nikiwa kiongozi mwenye dhamana ya kusimamia masuala ya Utumishi wa Umma nchini, ninazielekeza taasisi za umma kuitumia kauli mbiu hiyo wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2020 yanayoanza tarehe 16-23 Juni, 2020 kwa kutoa huduma katika taasisi zao, ikiwa ni pamoja na kuainisha namna taasisi zinavyoshiriki kujenga na kudumisha ushirikiano wa kiutendaji na wananchi na wadau ili kuweka mazingira wezeshi ya utoaji wa huduma bora na kwa wakati kwa kuzingatia Mikataba ya Huduma kwa Mteja.

Katika kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka 2020, kama ilivyokuwa maadhimisho ya mwaka jana, Ofisi yangu inawaelekeza Watendaji wa Taasisi za Umma, kuadhimisha wiki hii kwa kukutana na watumishi katika maeneo yao ya kazi ili kusikiliza maoni na changamoto wanazokutana nazo katika utekelezaji wa majukumu yao ikiwa ni pamoja na kukutana na wadau wa nje kwa lengo la kupata mrejesho wa huduma wanazozitoa, huku tahadhari dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa CORONA zikichukuliwa.

Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma wanapaswa kuhakikisha kuwa tahadhari dhidi ya Corona inapewa kipaumbele wakati wa maadhimisho kwa kufuata Miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya pamoja na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Nchi.

Katika kujenga mahusiano mazuri yatakayowezesha utendaji kazi wa taasisi za umma, taasisi zinaweza kuadhimisha wiki hiyo kwa kufanya shughuli za kijamii katika maeneo ambayo wananchi wanapata huduma (hospitali, sokoni nk.) kwa kuzingatia tahadhari dhidi ya Corona.

Mara baada ya kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, ninaziagiza taasisi zote za umma kuwasilisha taarifa ya namna walivyoshiriki maadhimisho hayo kwenye Ofisi yangu ili Serikali iweze kutumia taarifa hizo kufanya tathmini na kuboresha utendaji kazi.

Ni matumaini yangu kuwa, maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka huu yatatumiwa na watumishi wa umma nchini kujitathmini kama wanaendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Tano ambayo imedhamiria kwa dhati kuboresha huduma zitolewazo na Taasisi za Umma kwa wananchi na hatimaye kuwa na mchango katika maendeleo ya Taifa.

Mwisho kabisa lakini sio kwa umuhimu, nachukua fursa hii kuwapongeza watumishi wote wa umma nchini kwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo pamoja na changamoto za maambukizi ya Homa kali ya mapafu kuwepo. Kipekee tunaipongeza sekta ya Afya kwa kufanya kazi yenye changamoto nyingi katika kipindi nchi ilipopita katika janga la maambukizi ya COVID-19.

Kwa jumla nipende kuwahakikishia watumishi wote wa umma kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inawathamini na iko pamoja nanyi, hivyo ninawahimiza kuendelea kuchapa kazi kwa manufaa na maendeleo ya taifa letu kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli anavyosisitiza kupitia kaulimbiu yake ya “**HAPA KAZI TU**” ambayo imekuwa ni chachu katika kuimarisha nidhamu ya utendaji kazi kwenye Taasisi za Umma.

TAREHE 14 JUNI, 2020